Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na unapowaona wale wanaozihafifisha Aya Zetu, basi ujitenge nao mpaka wazungumze maneno mengine; na kama Shetani akikusahaulisha, basi usikae baada ya kukumbuka pamoja na watu wadhalimu. (AL-AN'AAM 6:69)

JUZU 80 No. 212 | JUM.I-JUM.II 1440 AH | FEBRUARI 2020 | TABLIGH 1399 HS | BEI TSH. 500/=

Virusi vya Corona: Ni Janga au Ishara ya Kimbingu?

Na **Rajabu Abasi Mkieti**
Ikwiriri - Rufiji



Dunia ya leo inakabiliwa majanga makubwa ambayo yanapelekea kuangamiza watu na mali katika kila Nyanja. Hatari ya matishio yote hayo inaonyesho kuwa sayari hii ya dunia ambayo ilikadiriwa na Mwenyezi Mungu kuishi viumbe mbalimbali ikiwamo binadamu hivi karibuni havitaweza tena kuishi kwa usalama.Zipo sababu nyingi zinazo elezwa kuwa ndio vichochea vya majanga hayo.Mabadiliko ya hali ya nchi yana tajwa kuwa ni moja ya janga kubwa linaloongeza vifo vya watu kwa kupelekea na ukame na mvua zisizo za msimu zinazoleta mafuriko katika eneo kubwa la dunia,tishio la kuzuka vita ya tatu ya dunia likiongezeka.

Yote hayo yakishika kasi huku ufumbuzi wa suluhisho la majanga hayo ukiwa haujapatikana kirusi kipya cha Corona kinachoshambulia uhai wa binadamu kwa haraka sana nacho kimezuka nchini China katika mji wa Wuhun mashariki mwa nchi hiyo. Wataalamu wa afya dunia wanakiangalia kirusi hicho kwa mtizamo wa janga la kimataifa.Sawa na taarifa zilizo tolewa na shirika la afya dunia WHO vifo vimeripotiwa kutokana na ugonjwa huo dunia na zaidi ya 900 hadi sasa wamesha fariki kutokana na ugonjwa huo. Ugonjwa huo umeshasambaa katika mataifa mbalimbali dunia. Aidha watu wanao fariki kwa siku kutokana na virusi hivyo vya corona ni zaidi ya watu 70.Kwa mujibu wa tume ya Afya nchini China vifo vingi vimeripotiwa katika mji wa Wuhan ndani ya jimbo la Hubei ambako ndiko chimbuko la ugonjwa huo uliozuka Desemba 2019 ,kwa mujibu wa shirika la afya dunia WHO zaidi ya watu 40600 wameripotiwa kuambukizwa virusi hivyo vya corona dunia.

Nchi ya mbalimbali dunia ikiwamo China tayari zimesha chukua hatua mbalimbali za dharura kupambambana na ugonjwa huo ikiwamo kuwaweka watu ambao wamesha ambukizwa katika sehemu maalumu .Wanasanyansi wa afya wanapata wasiwasi zaidi kwani mtu aliyeathirika na virusi vya corona huanza kuambukiza watu wengine ndipo nayeye huonyesha dalili za kuonekana ameambuklizwa.Wasiwasi huo wa wanasanyanzi wa afya ndio unaowashinikiza kulazimika kuuona ugonjwa huu ni janga la kimatifa.

Bila `shaka yanayotokea dunia yanatuhitaji tutafakari zaidi je

Endelea uk. 2

Kozi ya Kihistoria ya Makatibu wa Waqf e Nau



Na **Amiri Kaluta Abedi**
Dar es salaam

Kwa Msaada mkubwa wa Allah Kozi ya kwanza ya kihistoria ya Kimataifa ya Makatibu wa Waqfu Nau Duniani ilifanyika huko Uingereza kuanzia tarehe 6 hadi 8 Disemba 2019. Alhamdullillah.

Kozi hiyo iliandaliwa na Mudiri wa Idara ya Waqkfu Nau Markaz ya Jumuiya huko London Uingereza Bwana Luqman Ahmed Kishwar na kupata baraka zote za Mtukufu

Endelea uk. 4

Adamu: Nabii na Si Kiumbe cha Kwanza

• Mwisho wa Mchakato wa 'Evolution' Ndio Zama za Adam

Na **Juma Iddy Abeid, Kigoma**

Ukitazama vitabu vya Biblia na Qur'an kwa makini utaona tofauti kubwa ya masimulizi yanayo muhusu Nabii Adam[as] maana masheikh na wachungaji humfanya kuwa ndio mtu wa kwanza kuumbwa na Mungu.Mafundisho hayo yanapingana na vitabu hivyo viwili, kwani mtu alipitia katika mchakato wa taratibu mbali mbali. Kwani kuna aya ndani ya Qur'an ambazo zinaonyesha kwamba uumbaji wa mwanaadamu (MTU) ulikuwa wa mwisho wa kimchakato wa taratibu.

Kwa mujibu wa Qur'an tukufu, mtu hakuumbwa ghafla kwa kipindi kimoja. Na ndio maana Qur'an imezungumzia mtu kuumbwa kwa namna nyingi kama upatikanaji wake.

Qur'an 21:31: *Je, hawakuona wale waliokufuru ya kwamba mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana kisha Tukaviambua; na Tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai; basi je, hawaamini?*

Aya hii inahusu watafiti wa maumbile ya viumbe ambao Qur'an ilionesha zama zitafika za kuchunguza vyanzo mbali mbali. Watafiti hao ndio waliogundua maji ndio matokeo ya Hydrogen na Oxygen.

Wanasema ukiutazama mwili una Hydrogen 10% Oxygen 65%

Endelea uk. 4

Somo Kutoka kwa Moi uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Somo Kutoka kwa Moi

Utatembea sana katika kurasa za historia kutafuta kiongozi anayependwa sana na watu, aliyekamilika. Utakachofanikiwa ni kutompata kiongozi huyo! Na hayupo. Tunachokifahamu anapofariki mtu ndipo tunaeleza tena kwa mishipa kututoka mazuri aliyoyafanya. Naye mwandishi maarufu wa Uingereza anakumbusha, “maovu wayatendayo binadamu huishi wakishakufa, mema huzikwa pamoja nao”. Hayo yote tunayatilia maanani isipokuwa muktadha wetu hivi leo ni nini tunaweza kujifunza kutoka kwa aliyewahi kuwa Makamu wa Raisi na Rais wa Kenya kwa miaka ishirini na nne, Daniel Arap Moi?

Daniel Arap Moi ni shahidi kuwa penye nia pana njia na daima uwe na shabaha maishani. Daniel Arap Moi alianza akiwa Mwalimu wa shule ya msingi. Aliipenda, kuiheshimu na kujivunia kazi hiyo. Aliifanya kazi hiyo kwa kujituma na mapenzi makubwa. Alisumbuka sana alipomuona mwanafunzi wake hajaelewa. Hapo alitafuta mbinu na mikakati ya kumuelewesha. Furaha na tabasamu lilitawala uso wake mara alipoona wanafunzi wake wameelewa. Kazi hiyo aliendela nayo hadui alipokuwa Rais wa nchi na kuwafundisha Wakenya wenzake faida na manufaa ya amani, mapenzi na umoja.

Katika hili tunajifunza kuwa ni lazima toka mwanzoni kabisa tufanye uamuzi ni kazi gani tunayotaka kufanya maishani, tukishachagua tuipende na kuiheshimu kazi hiyo tuliyoichagua kwa manufaa ya taifa. Watu wengine hawawezi kuheshimu kazi yako kama wewe kuiheshimu. Kazi yaualimu ndiyo kazi ya Mitume, kuleta nuru palipo giza. Katika Afrika kazi hii ya ualimu imetupatia mashujaa wetu akina Kwame Nkurumah, Kenneth David kaunda, Julius Kambarage Nyerere na Daniel Arap Moi.

SISI NI WA ALLAH

Napokea simu. Ni majira ya saa kumi na moja. Kwa huzuni Maulana Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya ananipatia taarifa Mwalimu B. K. Heri katutoka duniani. Napokea kwa kumuambia sisi ni wa Allah na kwake tutarejea.

Mwalimu B. K. Heri nilifahamiana naye toka 1965 miongoni mwa wasomi wa mwanzoni kujiunga na Jumuiya. Mpole na ambaye daima ana kitabu chake anasoma - hulka ilinivutia sana. Ilipunguza muda unaotumiwa katika kupiga porojo. Aliheshimu muda na akautumia vizuri. Chuo cha Wabashiri kilipoanzishwa Masjid Salaam chini ya Sheikh Kaluta Amri Abedi, yeye alikuwa ni mwalimu wa Kiingereza. Aliifanya kazi hiyo kwa bidii na mapenzi makubwa. Wakati akifundisha aliendelea kutoa makala katika Mapenzi ya Mungu, makala nzito zinazopatikana katika Mapenzi ya Mungu ya miaka ya hamsini.

Kuna kipindi aliitumikia Jamaat katika wadhifa wa kuhariri gazeti la Mapenzi ya Mungu. Gazeti lilitoka kwa wakati na kuhakikisha kutokuwepo na makosa ya uchapaji.

Tunamuombea kwa Allah juhudi yake hiyo ipokelewe ili ahesabiwe miongoni mwa wale waliotumia kichwa na kalamu katika kuzagaza nuru ya Islam.

Virusi vya Corona

Kutoka uk. 1

kuna bishara za kumbingu iliyo tabiri kuzuka kwa majanga haya.Kama kweli ukitafakari ukiwa muumini na mfuasi wa dini yoyote ile mara moja utagundua kua hizi ndizo

Mwanadamu anawezaje kukimbia kutoka kwa Mungu Ambaye mikononi Mwake vomi vitu vyote" (Tajalliyat-i-Ilahiyah, Ruhani Khazain, Juz. 20, uk. 396)

Atawalindeni. Mkiwa mmeghafilika juu ya adui zenu Mwenyezi Mungu Atawaangalieni na Atavunja hila zao. Mpaka sasa hamjajua uwezo wa Mungu wenu, lau kama



Wataaalamu wa afya wakidhibiti mazingira aliyofia mtu kwa virusi vya Corona

zama za ujio wa mara ya pili wa Yesu kristo au Isa bin mariam. Zaidi ya miaka 110 iliyo pita,Hazrat Mirza Ghulam Ahmadi as wa Qadian alidai kuwa yeye ndio Masihi aliyeahidiwa na amekuja kutimiza ujiwa wa Yesu mara ya pili.Sawa na bishara hiyo alidai ukweli wake umeambatana na kutimia kwa ishara mbalilmbali ikiwamo tauni,njaa ,ukame ,matetemeko ya ardhi pamoja na majanga mabalimbali.

Maelezo yanayopatikana katika Biblia yanaonesha kudhihiri kwa Yesu as kwa siku zijazo ni zitakua za majana kama inavyoelezwa katika Mathayo 24:4 “kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali”.

Hazrat Mirza Ghulam Ahmadi[as] wa Qadian alidai kuwa majanga hayo ya maradhi na matetemeko ni kutoka kwa Allah ikiwa ni alama za ujio wake wakati wakudhihiri na baada ya kudhuhiri.

Masihi Aaliyeahidiwa[as] anasema ***“Kama tabiri hizi zikileta utisho mkubwa duniani wakati wa kutimia kwake na kuwachanganya watu kutokana na wingi wa taharuki au kuziletea hasara miundombinu na maisha katika maeneo mengi basi mwogopeni Mungu ambaye Amefanikisha haya yote kwa ajili yangu.***

Kwa hakika virusi vya Corona japo kuwa ni ugonjwa lakini pia ni alama za kutaka watu watafakari kuwa sasa mtu aliyekuwa akisubiriwa duniani ameshafika njia pekee ili dunia ipate usalama ni kuungana naye ili Mungu wetu Atulinde katika majanga na madhila mbalimbali katika dunia hii.

Masihi Aliyeahidiwa[as] anasema ‘Kama ninyi mtakuwa wa Mungu, fahamuni kwa yakini kuwa Mwenyezi Mungu pia Atakuwa wa kwenu. Mkiwa mmelala, Mwenyezi Mungu ninyi mngalijua uwezo wa Mungu wenu, lau kama ninyi mngalijua haya isingetokea siku yoyote ninyi kuhuzunikia dunia yenu’ (Safina ya Nuhu uk 15. chapa ya nne 1987)



Kuvaa vitu vya kuzuia pua na mdomo, kuwakusanya wataalamu wa afya na kutafuta dawa hizo ni njia za muda mfupi tu. Kwa maneno hayo ili tuokoke na janga hili la virusi vya Corona bila shaka njia iliyo sahihi na ya kudumu ni kumpokea mjumbe wa zama hizi ili atuunganishe na Mola wetu Mlezi.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Hadhrat Amman Jaan[ra]

Na Sheikh Abid Mahmood Butt
Jalsa Salana Tanzania 2019

Kutoka toleo Lililopita

Alivyodumu Katika Ibaada Maishani Mwake.

Kama ilivyo kwa wanawake wengine wa kawaida Hadhrat Nusrat Jehan Begum sahiba[ra] alikuwa na majukumu mengi ya nyumbani kama vile kupika kufagia kufua nguo na kuzishona pindi zilipo chanika, kuogesha watoto na kadhalika. pia alikuwa na familia kubwa ndugu wa pane zote mbili, wageni, alitembelea wajane, yatima, maskini pamoja na wanfunzi.hata hivyo alioonyesha na kuthibijsha kwamba majukumu ya nyumbani hayawezi kuwa kikwazo kwa mtu katika kutekeleza ibaada ya Allah.
Hadhrat Mirza BAshir Ahmad sahib[ra] (abaye ni mmoja wa watoto wake wa kiume) akielezea uchamungu wa mama yake anasema :

"Ni vigumu kueleza kwa maneno machache juu ya ucha mungu wake, kwani ilikwa ni kawaida yake kusali sala zote tano kwa wakati wake na kwa shauku kubwa sana, pia alikuwa akisali sala za nafali ikiwemo pia sala ya tahajud ambayo aliisali kila siku. Hali yake ya sala ilikuwa i ya kustajabisha sana,pindi alipokuwa kwenye sala, alisali kwa shauku kiasi kwamba kila aliyekuwa naye katika sala aliathirika sana."

Hadhrat MIrza Bashir Ahmad[ra] anaendelea kusema kuwa ile hadithi ya mtume mtikufu[saw] isemayo kuwa "Furaha ya macho yangu imo katika sala." ilithibithika na kudhihirika kwa Hadhrat Amma Jaan[ra]. zaidi ya sala mama huyu mtukufu alidumu kufanya maombi mbalimbali maishani mwake. Alikuwa na kawaida ya kuwaombea wafanyakazi wa jumuia na wana jumuia wote kwa jumla na pia aliwaambia wanajumuia wamwombee na hasa watoto, kwani alisema watoto hawana dhambi na hivyo maombi yao yanapoikelewa haraka na Allah.
Hii inaonyesha jinzi Hadhrat AMma Jan alivyokuwa na ikhilasi ya hali ya juu kabisa, kwani pamoja na hadhi, heshima na taqwa aliyokuwa nayo lakini hakutaka kabisa kujikweza.
Inasimuliwa kuwa mwanamke mmoja alivyopaya mtoto (binti) wakwanza, alimwendea Hadhrat Amma Jaan na mwanaye. Na muda wa sala ulipofika, Hadhrat Amma Jaan[ra] aliendelea kusali na aliporudi aliwauliza mabindi (wakubwa) waliokuwepo hapo nyumbani wakati huo, jee mmesali? yul;e mamam mtoto aliyekuja kupata maombi akajibu akasema "mtoto amenikojolea hivyo nitenda kusali nyumbani baada ya kupata twahara na kubadilisha nguo".
Hazrat Amma Jaan[ra] sahiba aksema,mtoto asiwe sabau ya kutosali kwa wakati,aliongeza kusema kuwa watoto ni zawadi kutoka kwa Allah,hivyo haimpasi kutoa kisingizio kupitia katika zawadi ya Allah.
Hii inatuonyesha ni jinsi gani Hazrat Amma Jaan[ra] alivyojali na kuthamini muda wa sala na namna gani alikuwa makini katika utekelezaji wa Ibada.

Maombi Yake Mbalimbali

Kama nilivyoeleza hapo juu ya kwamba Hazrat Nusrat Jahan Begum sahiba[ra] alipenda sana kuomba dua kwa wingi katika maisha yake na kuwaomba wengine wamwombee.
Inasimuliwa kuwa mama huyo alipohamia Rabwa ,pamoja na dua nyinginezo,pia aliomba sana dua hii:-

Rabbi kullu shain khaadimuka Rabbi fakhfidhni wansurni warhamni

Aliwafundisha wtoto dua hii na kuwaamuru waisome kila mara na akasema;
"Hii ndio dua kuu katika zama hizi".
Inaelezwa kuwa mama mmoja alienda kwa Hazrat Amma Jaan[ra]na kumuomba ruhusa ili akasali katika kile chumba maalum ambacho Hazrat Masihil mau'ud[as] alikitumia kwa kufanya maombi maalum tena kwa wingi (Baitud-duaa). Hazrata Amma Jaan[ra] akajibu kwa kusema "Hatujaweka kodi ya kuingia humo", akiwa na maana kwamba mama huyo anaruhusiwa kuingia humo na kufanya maombi humo. Wakati mama huyo mgeni alipokuwa anataka kuingia, Hazrat Amma Jaan[ra] akamwaambia, "naam kuna kodi moja imewekwa, nayo ni hii kuwa nakuomba uniombee na mimi pia."

Hadhrat Amma Jaan[ra] Alikuwa na Mapenzi ya Dhati Juu ya Allah, Kitabu Chake Na Mtume Wake[saw]

Mapenzi ya Hazrat Sayyida Nusrat Jahan Begum sahiba[ra] juu ya Allah, Quran tukufu na Mtume mtukufu[saw] ni ya aina ya pekee sana.
Wanajumuiya wengi wanasimulia kuwa Hazrat Nusrat Jahan Begum[ra] kila alipopata tatizo au huzuni au hata alipomkumbuka Masihi aliyeahidwa[as] basi yeye alichukua Qurani tukufu na kuanza kusoma.
Katika simulizi nyingine inasimuliwa kuwa kila alipopata shida alikuwa akisoma *Suurat yaasin* (sura ya:36 katika Qurani tukufu)na alisema "sijui ni kwanini watu(waislamu) wameihusisha surah hii na kifo tu,ilhali Masihi Aliyeahidiwa[as] alisema,"katika wakati wa kila shida kama mtu atasoma surah *yaasin*,basishida hiyo itatoweka.

Mapenzi Yake Juu ya Hadithi

Kama tujuavyo kwamba Hazrat Masihil mau'ud[as] amezielezea hadithi kuwa ni njia ya tatu ya mwongozo baada ya Qurani Tukufu na Sunna za Mtume[saw] .
Hazrat Amma Jaan sahiba[ra] katika kuziheshimu,kuzipenda na kufanyia kazi hadithi za Mtume[saw] mfano wake ni wa pekee .Kwa mfano inasemwa kwamba mama huyu alikuwa na kawaida ya kumwita mtu (mwanajumuiya) ili amsomee hadithi na yeye alisikiliza kwa makini sana na kwa muda mrefu .Huu ulikuwa ni wakati ambao alizeeka sana na alipenda kuwatumia mayatima wa kike aliowalea mwenyewe.
Katika tukio lingine inaelezwa kuwa mfanya biashara mmoja alitaka kukodi shamba la miembe ya Hazrat Amma Jaan[ra] (kama ifanyikavyo katika sehemu mbalimbali katika jamii mbalimbali duniani) wakati huo miembe ilikuwa imeanza kutoa maua na baado ilikuwa haijabeba matunda,mtu huyo alikuwa tayari kulipa rupia 600 pesa ambayo ilkuwa ni nyingi sana ,lakini Hazrat Amma Jaan[ra] alikataa akisema "utaratibu huo ni kinyume na mafundisho ya Mtume[saw] .
Yaani kama itakumbukwa kuwa Mtume[saw] alikataza wafanyabiashara wasiende kwa wakulima kununua mazao bali waache yafike sokoni.
Embe zilipokuwa tayari na kuuzwa,thamani yake haikufikia rupia 600 ambazo alitaka yule mnunuzi wa kwanza .Mtu huyo aliyetaka kununua mwanzo alimwendea msimamizi wa mashamba hayo na akasema"mimi nilitaka kutoa pesa nzuri (nyingi) ninyi mlikataa,mnaona sasa mmepata hasara ".Yule msimamizi wa mashamba akasema "kivyovyote vile Hazrat Amma Jaan[ra] asingekubali kukuuzia kwa utaratibu ule ,na kupuuza mafundisho ya Mtume[saw].
Riwaya hii inatuonyesha jinsi Hazrat Amma Jaan Sahiba[ra]. alivyokuwa makini kusoma hadithi na kuzifanyia kazi.

Kuwajali Wafungwa

Qurani tukufu inasema;-
"Na huwalisha chakula maskini na yatima na wafungwa kwa mapenzi yake." (79:9).
Katika kutekeleza fundisho hili, Hazrat Amma Jaan Sahiba[ra]. mfano wake ni wa kusisimua.
Inasimuliwa kuwa safari moja alienda Batala na akamwuliza Dr.Hashmatullah sahib kama inawezekana kupata kibali cha kulisha wafungwa na akamkabidhi mama huyo – Dr.Hashmatullah Sahib jukumu la kufuatilia kibali. Na kibali kilipopatikana Hadhrat Amma Jaan[ra] akampa D. Hashmatullah sahiba rupia 50 {hamsini} ili anunue na kuandaa chakula kizuri kwa ajili ya wafungwa. Wafungwa walikula na walifurahia sana {inasemekana kuwa wafungwa hao ni wale walioshindwa kulipa madeni yao}.
Tukio hili linatuonyesha jinsi Hadhrat Sayyida Nusrat Begum Sahibah[ra] alivyokuwa mnyoofu katika kutekeleza mafundisho ya dini tukufu ya Islam._

Mambo Aliyoyachukia Maishani Mwake

Qurani Tukufu imekataza na kukemea mambo mengi kama vile kuteta,kusengenya,n.k (49:12-13).
Inasemekana kulikuwa na mama mmoja aliyekuwa na tabia hizo.Hazrat Amma Jaan[ra] aache tabia hiyo sio nzuri.Mama huyo akasema,"amekwambia mwanamke fulani? Akataja na jina la mwanamke huyo.Hapo Hazrat Amma Jaan[ra] akakasirika sana na kumwambia,nimekwambia ili urekebishe,badala yake unaleta dhana mbaya juu ya mtu mwingine!

Imani Yake Juu ya Hazrat Masihil Mau'uud[as]

Imani ya Hazrat Amma Jaan sahib juu ya Masihi aliyeahiiwa[as] ilikuwa ni ya kiwango cha juu kabisa,mifano michache ifuatayo inathibitisha jambo hili:-
(*a*) Kama itakumbukwa kwa Masihi Aliyeahidiwa[as] wakati wa uhai wake aliwahi aliwahi kwenda Lahore na huko alikaa siku kadhaa katika nyumba ya wanafamilia wa Hazrat Amma Jaan[ra].Baada ya kifo cha Hazrat Masihil mau'ud[as] siku moja Hazrat Amma Jaan[ra]alienda Lahore ili kuwasalimia ndugu na jamaa. Mmoja wa wanafamilia alimwambia Hazrat Amma Jaan[ra],"utuombee ili tupate nyumba kubwa".Yeye alijibu kwa kusema "msiidharau wala msiiache nyumba hii kwani Hazrat Masihil mau'uud alikaa humu ,hivyo hii nyumba si ndogo".
(*b*) Hazrat Masihil mau'ud[as] alipopata ufunuo kutoka kwa Allah kuhusu Ahmad beig ambamo ndani yake kulikuwa na bishara ya kumwoa binti yake muhammadi begum pia. Hadhrat Masihi mau'ud[as] alitangaza ufunuo huu ikiwemo kuhusu utabiri wa kumwoa binti huyu. siku moja Hadhrat Masihi MAUD[as]. alimwona hadhrat amman jaan[ra]. akifanya maombi kwa unyenyekevu mkubwa ktk sala yake chumbani mwake.alipomaliza kusali Hadhrat Masihi maud[as].alimwuliza ulikuwa unaomba nini,akajibu nilikuwa naomba kuhusu kutimia kwa utabiri huu. akamwambia je huogopi changamoto zitakazoambatana na kutimia kwa ufunuo huu?"(yaani kupata mke mwenza).Hapo Hazrat Amma Jaan[ra] akasema,vyovyote itakavyokuwa iwe,la muhimu utimie utabiri wa Allah na maneno yako,furaha yangu imo katika kutimia kwa utabiri huu".Kwa kawaida wanawake huwa hawapendi kabisa kuolewa mitala,lakini hali imekuwa tofauti kabisa kwa Amma Jaan[ra] kama tulivyoona hapo juu.
(c) Katika uhai wake Masihi Aliyeahidiwa[as]. licha ya kutamani sana hakubahatika kufanya ibada ya hijja kutokana na sababu mbalimbali.Hadhrat amman jaan[ra] alikumbuka sana tamanio hili la hadhrat Masihi maud[as].,hivyo mama huyu akatoa pesa na kumpa mtu mmoja ili akafanye hijja badala ya Hazrat Masihil mau'ud[as].
(*d*) Kila alipomkumbuka Hazrat Masihil mau'ud[as],Hazrat Amma Jaan alichukuwa Qurani Tukufu akasoma na kumwombea dua. Na pia alikuwa anaenda kaburini alikozikwa Masihi Aliyeahidiwa[as] na kumwombea dua.
Mifano hiyo michache na mingine mingi inatuonyesha ni kwa jinsi gani Hazrat Amma Jaan[ra] alivyokuwa na imani thabiti juu ya Masihi Aliyeahidiwa[as] na ujumbe wake,na pia inatuonyesha ni nini sababu ya kumteua na kumwandaa mama huyu kuwa mke wa mjumbe wake.
Hali yake ya imani juu ya hadhrat Masihi maud[as] inatukumbusha hali ya imaani ya hadhrat khadija[ra]. juu ya mtume mtukufu[saw].

Itaendelea toleo Lijalo

Kozi ya Kwanza ya Kihistoria ya Makatibu wa Waqf NauDuniani Yafanyika Uingereza

Kutoka uk. 1

Khalifatul Masih V (atba).

Tanzania iliwakilishwa nami nikiwa ni Katibu wa Waqfu nau Taifa. Nchi zingine zilizohudhuria ni pamoja na Gambia, Ghana, Nigeria, Congo na Siera Leone na Mauritius. Zingine ni Marekani, Canada, Newzealand, Sweden, Bangladesh, Malaysia, Urusi, Australia, Switzerland, Uholanzi, na Uingereza.

Hazur (atba) aliwahutubia Makatibu tarehe 7 Disemba, kupiga nao picha ya pamoja na kisha kula nao pamoja chakula cha jioni.

Kwa Muhtasari Hazur (atba) alisema yafuatayo:-

1. ***Makatibu wa Waqfu nau wana jukumu kubwa la kuhakikisha malezi ya watoto wa waqfu Nau na wasilichukulie suala hilo kiwepesi. Watoto hao watafanya kazi za Jamaat za Ubashiri, daktari ualimu na fani zinginezo hivyo ni muhimu wapate malezi mazuri.***

2. ***Kwa kuwa makatibu wa Waqfu nau ndio wenye jukumu la malezi ya watoto hao basi wao wenyewe ni lazima waongeze viwango vyao vya ucha Mungu na kujiweka saa zote karibu na MwenyeziMungu. Wakifanya hivyo bila shaka watapata matunda yanayotarajiwa na watoto wa Waqfu nau wataiga mifano yao. Hazur (atba) aliagiza makatibu wa Waqfu Nau kuzingatia sala za faradhi, sala za nafali na kufanya ibada kwa unyenyekevu wa hali ya juu.***

3. ***Ni jukumu la Makatibu wa Waqfu nau kuwaelekeza watoto wa waqfu Nau kwa namna iliyo bora kabisa na (Makatibu hao) hawawezi kutekeleza hilo bila kujijengea uhusiano imara na Allah.***

4. ***Makatibu wa Waqfu nau wanapawsa kuzingatia daima kwamba watu waliwaamini na kuwapendekeza wakati wa Shuura kuwa makatibu wa Waqfu Nau na Khalifa wa Zama amewapa jukumu hilo moja kwa moja. Jukumu hili wataweza kulitekeleza endapo tu watafuata mafundisho ya dini tukufu ya Islam katika kila hatua ya maisha yao.***

5. ***Makatibu wa Waqfu Nau wamepewa jukumu la kufanya malezi ya watoto kielimu ya kidin na kidunia. Hivyo Makatibu wa Waqfu na wanapaswa kuratibu mipango kwa kuzingatia hilo. Makatibu wa Waqkfu Nau wanapaswa kuwafahamisha watoto wa Waqkfu Nau kuwa 'waqfu –e-Nau" sio cheo cha heshima tu bali ni ahadi iliyo tukufu katika maisha yote. Mkifanikiwa kuwafundisha tabia hizi utotoni mwao ndipo watoto hao watatimiza ahadi zilizowekwa na wazazi wao wakati (watoto hao) watakapobaleghe, InshaAllah.***

Makatibu walipatiwa fursa ya kutembelea Jamia ya Uingereza ambacho ni Chuo cha kuwafundisha Mashekhe wa Jumuia, Markaz Tasweer ambacho ni kitengo cha picha za kumbukumbu za Jumuiaya na pia walipewa fursa ya kuzungumza na Mwandishi wa Hazur (atba).

Ninawaomba watoto wote wa Waqfu nau, Wazazi wote wa watoto hao na Wanajumuiya wote kwa ujumla kutuombea sana kwa Allah Makatibu wa WaqfuNau duniani ili Atuwezeshe kutekeleza majukumu yote kwa kiwango cha kumridhisha Hazur (atba) kwa asilimia mia moja, Amin.

Taarifa zaidi zitatolewa katika tolea lijalo inshaAllah.

Adamu: Nabii wa Kwanza Duniani, Si wa Kwanza Kuumbwa

Kutoka uk. 1

navyo ni vizalisho vya maji. Je mtu hategemei hivyo? Iwapo yeye akiwa anategemea inaonyesha katika kila chenye uhai nae alikuwa kama muhusika mkuu. Kwani ujumbe huo anapewa mtu ili apate kujielewa.

Pia aya hiyo zinatofautiana na nadharia ya THE BIG BANG ambapo waliamini ulimwengu ulipata mpasuko mkubwa wa tufe lilikuwepo wakati huo kabla ya haya maumbile tuliyo nayo sasa. Wakasema mpasuko huo ulitokana na joto kali.

Katika tukio hili lilikuwa chanzo juu ya uhai wetu. Uhai ambao ausishwi Nabii Adam a.s. Je, kwanini tunasema watu walianzia hapo kabla ya Adam sababu mtu ni umbile tulilo nalo lenye sifa ya kutembea tukiwa tumesimama kwa kutegemea miguu miwili.

Qur,an inasema katika sura NUHU 71 AYA 18-19-:

Na Allah Akawaotesheni katika ardhi kama mimea: Kisha Atawarudisheni humo na Atawatoeni tena.

Kwa mujibu wa hizo mbili kwa kila mwenye kutafakari kwa kina ataona wazi kuwa watu waliumbwa kwa kuwepo ardhini, kwani hakuna mwislamu asieamini ufufuo wa pamoja ambao Mwenyezi Mungu amesema atatutoa tena.

Uumbaji huu hatuwezi kuunasibisha na uumbaji wa Adamu. Pia na hatuwezi kusema ni wa baada ya Adamu a.s. tukisadiki hivyo itakua tunaacha misingi ya aya nyingi za Uumbaji.

Na tusipozikwepa ni lazima kuukubali ukweli wa EVOLUTION kwa malengo ya Qur'an tukufu. Katika pendekezo nililolisema. Mfano kuna aya ndani ya Qur'an ambazo zinaonyesha kwamba uumbaji wa watu ulikuwa wa kimchakato wa taratibu na kwamba si sahihi kuwa Mwenyezi Mungu alimuumba mtu kutokana na udongo na kumpulizia roho yake.

Vitendo hivi viwili huisiwa tofauti, Qur'an inasema katika 71:15-: *"Hali yeye Amewaumbeni namna namna mbalimbali."*

Hapo inaonyesha wazi Allah Aliwaumba watu kabla ya Adam. Watu hao walipita hatua mbali mbali baada ya hatua na hali baada ya hali, na yote yalifanyika kabla ya Adam.

Kwa mantiki hiyo mtu hakuumbwa ghafla na upeo tuliokua nao leo, hali hii ilitayarishwa kwa kuwa mtu ni kiumbe aliyekua akingojea maelekezo ya Mola wake. Na ndio maana Qur'an sehemu mbalimbali Allah Ametumia neno kuumba ambalo humaanisha mwanzo wa tukio la uwepo wa kitu. Ikiwa na makusudio kila hatua ya upeo mpya ni sawa na uumbaji.

Watu hao wa awali wanaonyesha walikuwa hawana uwezo wa kubeba wajibu na majukumu na wajibu mzito wa sheria aliyofunuliwa Adam.

Watu hao walikuwa wakila matunda mbalimbali na kulala ktika mapango. Maisha yalikuwa magumu mno kutokana na mazingira yao, baridi kali, wadudu n.k Mwenyezi Mungu Aliwajaalia miili yenye manyonya na miili mikubwa yenye afya. Hakuna aliyewajua hadi zama za ugunduzi wa awali wa moto.

Qur'ani sura 76:2-: *Hakika ulimfikia mtu wakati fulani wa dahari ambapo hakuwa kitu kinachotajwa.*

Hapo inaonyesha mtu alikuwa hana historia ya maisha yake kwani hakuna aliekua anajua kusoma wala kuandika kumbukumbu zake. Jambo ambalo lilikuja vumbuliwa na watu wa baadae kua kulikuwa na zama za mawe baadae ilikua ni hatua pana.

Mtu alianza kupevuka katika zama za moto, kwani walitumia akili na bidi kubwa mno. Kama ni mfano wa ubwaji mpya. Watu hao walizidi kupevuka kutokana na vyakula vya aina mbali mbali kwa kuchoma na kupika. Walitambuliwa kama (Homohabilisi).

Qur'an ikawataja watu hao katika sura hiyo hiyo ya 76: 3-4: *Kwa hakika Tulimwumba mtu toka tone la manii lililochanganyika ambalo Tunalifanya lipitie katika majaribu; kisha Tukamgeuza kuwa kiumbe chenye kusikia na kuona.*

76:4 :- *Hakika Sisi Tukamwongoza njia awe mwenye shukrani au awe mwenye kukufuru.*

Hatua hiyo ya kujitoa katika maisha magumu ya kujificha kwa kukimbia baridi na kuishi kwa moto. Kurani ikawaita majini, jina ambalo linamaanisha uhalisia wa wale wanaoishi mbele kwa uficho.

Baadhi ya masheikh na waumini wao wanaonekana habari hii ya neno jinni kwa kutokulijua wakalitungia hadithi nyingi na visa vyao vya ajabu kwa kutoelewa kwao Qur'an. Lakini ukweli Qur'an haiwasaidii mahala popote katika hadithi zao hizo. Ukweli watu hao waliangaikia sana maisha ya dunia kwa kujihami na hali hiyo walitumia akili sana kwa hali ya juu Zaidi sawa na wakati wao huo.

Qur'an inaeleza wazi kwamba wakati huo ndipo Mwenyezi Mungu alipomtuma Adam a.s, katika wakati huo alikuepo mtu mmoja akiitwa kwa jina la IBILISI. Mtu huyo wataalamu waliowaita Homohabilis. Jina ambalo alitofautiani na jina lililopo ndani ya Qur'an tukufu. Huyu alikuwa mpinzani wa Nabii Adam a.s kama Abu Jahali kwa Mtume Muhammad s.a.w.

Mtu huyo ndio maana humkuti katika Qur'an mahali pengine popote nje ya kutajwa kwa Adam a.s. Na hatukufunzwa dua ya kujikinga na IBILISI ila shetani. Adam na watu wake walipo kwenda nje ya bustani ambayo tena kwa mujibu wa Qur'an ilikuwa ni eneo la dunia hii. Na sababu ya Mwenyezi Mungu kuwafukuza ni kwamba aliwaonya dhidi ya ibilisi ambae alikuwa mmoja wa majini. Na akawaambia wawe waangalifu yeye na watu wake. Adam na watu wake pamoja na ibilisi na watu wake walikuwa wapinzani wakubwa.

Qur'an inaonyesha katika sura 2:39 inaonyesha kwamba majini ya wakati wa Adam ambao ni watu wajuzi, wenye akili ma kiongozi wao IBILISI walikuwa katika zama zake wakati huo. Ndio kusema wale ambao kurani inaelezea kama majini kuhusiana na Adam walikuwa wanaadam kama wao wakagoma kuwa wanaAdam, yaani wafuasi.

Kama vile Qur'an inavyowaita Bani Israila. Majini wao waliamini kama muongozo ungekuja kutoka kwa Mwenyezi Mungu ungefikia miongoni mwao, kutokana na uwezo mkubwa wa akili yao. Hawakuamini kama Nabii Adam alikuwa mkamilifu zaidi yao.

Ufunuo ulishuka kwa sheria chache za kijamii kama kanuni ya kuishi na mahusiano yanayohusiana na malezi ya jamii na utumiaji wa chakula. Wale ambao akili zao za kijamii zilikuwa bado hazijaendelea kutengenezwa walikataa kujitoa kwa Adam. Mwenyezi Mungu akawaadhibu na kumpa Nabii Adam ushindi juu yao. Hapo ndipo mwanzo wa mgawanyiko wa silsila mbili na sifa tofauti yaani -: waaminio na wadhalimu.

Wadhalimu walimtegemea **Ibilisi** – Jina **Shetani** – Sifa ya kuwatelezesha wengine Na **Jini** sifa ya akili, Maarifa kufanya mambo kwa siri.

Mtu – Umbile alilokuwa nalo mwanadamu ni sifa ya ufuasi – wa kuzaliwa kiroho.

Itaendelea toleo Lijalo

Maadhimisho ya Mwana Aliyeahidiwa Yafana Jamia



Kwa msaada maalum wa Allah na baraka za khilafat,wanatawi wa Jamia Ahmadiyya waliadhimisha siku ya Muslih Mau'ud r.a katika tarehe husika kwa mujibu wa historia na kalenda ya Jama'at (yaani tarehe 20 February).

Kama ilivyo ada na taratibu za Jumuiya,hafla ilifanyika chini ya mwenyekiti Maulana Sheikh Ahmad Daud Mmoto sahib na ilianza kwa usomaji wa Quran tukufu ambayo ilisomwa na ustadh Salim Omar na kufuatiwa na shairi la ki-urdu lililosomwa kwa ustadi mkubwa na Ustadh Idrisa Juma.

Baada ya shairi hilo kilifuatia kipindi cha usomaji wa bishara kumhusu mwana wa ahadi,kazi ambayo ilifanywa na Ustadh Shukuru S. Magana sahib.Baada ya usomaji wa bishara,ilifuata hotuba iliyokuwa na maudhui yasemayo "Muslih Mau'ud r.a atajazwa na elimu ya ndani na nje".Hotuba hiyo ilitolewa na Ustadh Hashim Ntenje sahib.Ustadh alieleza muhtasari wa maisha ya Hadhrat Muslih Mau'ud r.a kabla ya kuanza rasmi hotuba yake.Kisha Ustadh alieleza kwa mapana na marefu juu ya jinsi gani bishara hiyo ilivyotimia kwa Hazrat Mirza Bashiruddeen Mahmud Ahmad r.a.Alitaja baadhi ya kazi muhimu alizopata kufanya mwana wa ahadi katika uwanja wa dunia na dini na kuthibitisha pasi na shaka yoyote kutimia kwa bishara hiyo juu yake.

Kilele cha hotuba hiyo kulitoa nafasi ya kusomwa kwa shairi la Kiswahili ambalo lilisomwa naye Ustadh Abdul-kareem Y.Mgeleka. Kisha ilifuata hotuba iliyokuwa na kichwa cha habari kisemacho, "bishara zimetimia" ambayo hotuba hiyo ya kusisimua iliwasilishwa na Mwl.Kassim A.Mgalu sahib. Mwalimu alifafanua kwa kina kutimia kwa bishara zinazomhusu mwana aliyeahidiwa juu ya Hazrat Khalifatul Masih II r.a. Mwishoni mwa hotuba yake ,mwalim aliwahimiza wasikilizaji kusoma vitabu vya Masih aliyeahidiwa a.s na vitabu vingine vyote vya Jamaat ili kufaidika na mafundisho mazuri yaliyomo humo.Na pia aliwasisitiza wasikilizaji kusikiliza hotuba ya khalifa mtukufu (atba) na kuangalia MTA .

Baada ya hotuba hiyo ilifuata hotuba iliyobeba ujumbe usemao "jinsi Mwana aliyeahidiwa r.a alivyoimarisha nidhamu ya ukhalifa katika Jumuiya". Hotuba hiyo adhwimu ilitolewa na Maulana Sheikh Azeez A.Shahzad sahib. Aliwakumbusha wasikilizaji matukio mbalimbali yaliyojiri katika zama za Khalifatul Masih II r.a na kupelekea mpasuko mkubwa katika Jumuiya ambapo viongozi wakubwa wakubwa walijitenga na ukhalifa na kuchukua pesa zote za Jumuiya na kwenda nazo Lahore.Alisema,kutokana na hali hiyo,Jumuiya ilikabiliwa na hali ngumu kiuchumi lakini kutokana na Baraka za Muslih Mau'ud r.a alisimama imara na kuivusha Jumuiya katika majaribio mengi makubwa na madogo.Hakika ilikuwa hotuba nzuri na ya kuvutia.



Sh Abid Mahmood Bhatti
Mkuu Jamia Ahmadiyya.

Hiyo ilikuwa ndiyo hotuba ya mwisho kwa siku hiyo kwani baada ya hapo mgeni rasmi ambaye pia alikuwa ndiye mwenyekiti wa kikao hicho Maulana Sheikh Daud Mmoto sahib alisimama na kutoa nasaha chache.

Katika nasaha zake Sheikh sahib aliwakumbusha wasikilizaji maagizo ya Hazrat Khalifatul Masih V (atba) yakuwa dhumuni la kuadhimisha siku muhimu katika Jumuiya ni kuvikumbusha vizazi vyetu historia ya Jumuiya kutoka kule tulikotoka,hapa tulipo na kule tuendako.Alisema hili ni jambo muhimu sana kwetu ili tusije kupoteza historia ya Jamaat na taswira yake nzuri. Mwisho mgeni rasmi aliwaasa wasikilizaji kuyafanyia kazi yale yote waliyoyasikia katika mkutano huo. Kisha aliongoza maombi ya kimya na kufunga kikao. Baada ya hapo sala ya Adhuhuri na Alasiri zilisaliwa kwa pamoja na kisha kupata chakula cha pamoja.

Mahafali ya 21 Jamia Ahmadiyya Yang'aa

- **Amir Jamaat awa mgeni rasmi.**
- **Katibu Elimu Kata na Mtendaji nao wahudhuria.**



Kwa fadhili za Allah na kwa Baraka za maombi ya Hazrat Khalifatul Masihil-khamis a.t.b.a wanachuo wa Jamia Ahmadiyya Tanzania walifanya mahafali yao ya 21 kwa ufaulu mkubwa-Alhamdulillah.

Mgeni rasmi katika mahafali hayo alikuwa ni Maulana Sheikh Twahir Mahmood Chaudry sahib-Amir na mbashiri mkuu wa Jumuiya ya waislamu waahmadiyya Tanzania.

Katika mahafali hayo wageni mbalimbali walialikwa na kuhudhuria wakiwemo wabashiri wa mikoa ya Mbeya, Iringa, Dar es salaam, Morogoro nk. Na pia viongozi mbalimbali wa serikalini akiwemo mwenye kiti wa mtaa,afisa mtendaji wa kata,mratibu wa elimu kata na wengineo nao pia walialikwa na kuhudhuria.Sambamba na hao,walikuwepo pia na waalimu wa shule ya Ahmadiyya Pr.School.

Hafla zilianza saa 4:30 asubuhi kwa usomaji wa Quran Tukufu ambayo ilisomwa na Usatdh. Salim Omar na kufuatiwa na shairi la kiurdu na tafsir yake kwa Kiswahili ambalo lilisomwa na Ustadh Sultan Amri Juneid.

Baada ya hapo ulifuata usomaji wa ripoti ya chuo kwa mwaka 2019 kwa lugha ya kiurdu ambayo ilisomwa na Maulana Sheikh Azeez A.Shahzad sahib na kufuatiwa na ripoti hiyo kwa lugha ya Kiswahili.Aidha ripoti hiyo ilionyesha kazi mbalimbali zilizofanyika mwaka wa 2019 kuanzia darasani hadi mazingira ya nje.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo,jumla ya wahitimu ni saba ambapo wawili kati yao ni kutoka Kenya na watano ndio watanzania.Sambamba na hao pia wanafunzi wawili wa darasa la kuhifadhi Quran Tukufu nao wamehitimu,hao ni:-Shadadi Saidi na Twahir Saidi Uthman-Alhamdulillah.

Kwa ujumla ripoti inaonyesha mafaniko makubwa ya Jamia katika Nyanja za masomo,Tabligh,michango,kazi za kujitolea-(waqar e amal),mashindano mbalimbali ya kimwili na kielimu,mahusiano mazuri na jamii nk.

Baada ya hatua hatua hiyo ,mgeni rasmi alitoa zawadi kwa wa kada mbalimbali kama vile wanafunzi wa shule yetu ya Ahmadiyya Pre. Primary School walioshika nafasi za kwanza na pili katika mitihani, wanafunzi wa Jamia Ahmadiyya walioshika nafasi za kwanza katika mitihani, wanafunzi walioshindana katika mashindano ya kielimu, mwanafunzi bora nk. Zawadi pia zilitolewa kwa wageni mbalimbali waalikwa na mwisho wahitimu walikabidhiwa vyeti vyao.

Baada ya hapo,Mgeni rasmi (Amir sahib), alitoa hotuba fupi kama nasaha kwa wahitimu. Katika nasaha zake Amir sahib alisema, leo ni siku ya furaha ya aina yake, kwani kwa mara ya kwanza tumejumuika pamoja na baadhi ya wanafunzi na waalimu wa shule yetu. Alisema tangu shule yetu imeanza miaka michache iliyopita imekuwa ikipata maendeleo siku hadi siku. Aliongeza kwa kusema kuwa, ni mpango wetu kujenga pia shule ya sekondari-Inshaallah. Pia alieleza kusudio la kuanzishwa kwa mpango wa Nusrat Jehan na mafanikio yake katika Afrika na hasa Afrika ya Magharibi.

Akiongelea juu ya wahitimu wa Jamia Ahmadiyya, Amir sahib alisema, bila shaka baada ya kuhitimu kwenu, Jumuiya itawapangieni majukumu katika matawi mbalimbali nchini. Mtakapokuwa huko, ninyi ni kama mabalozi wa Jumuiya katika maeneo hayo, hivyo ni lazima muoneshe taswira nzuri kwa watoto, vijana, wazee, kinamama na watu wote kwa ujumla ili kulinda heshima ya Jamaat.

Amesema kuwa wakati mwingine analazimika kuchukua hatua kali dhidi ya Waalimu ambao wanaharibu na kuchafua taswira ya Jumuiya. Amesema kuwa si kwamba anapenda kufanya hivyo, bali analazimika.

"Hebu fikirini kuwa Jumuiya inamhudumia kijana kwa miaka mine au na zaidi huku ikimgharamia chakula, malazi, matibabu,nk.Ni wazi kuwa Jumuiya inatumia gharama kubwa kwa ajili yenu na haiwezi kumsimamisha Mwalimu yeyote yule isipokuwa pale inapobidi" alisema Amir sahib.

Akasisitiza kuwaambia wahitimu ya kwamba jambo kubwa kabisa na la muhimu mara watakapopangiwa matawi yao, wafanye haraka iwezekanavyo kila mmoja wao apate ndoa.

Akasema, kama watachelewa kufanya hivyo basi yeye mwenyewe atachukua hatua kwa kuwasiliana na wazazi wao ili kukamilisha suala hilo.

Kisha akaongoza maombi ya kimya na kumaliza nasaha zake.

Baada ya nasaha hizo za Amir sahib lilifuata zoezi la upigaji picha za kumbukumbu, na kisha sala za Adhuhuri na Alasir zilisaliwa kwa pamoja na baada ya sala, wageni wote walikaribishwa katika chakula cha pamoja.

Bustani ya Washairi

WEKA AKIBA

Chochote takacho pata, usimalize kwa kula.
kidogo waweza kata, kukipeleka kwa mola.
na kingine tena kata, akiba weka mahala.
weka akiba swahiba, maisha yatabiriki.

Masihi Omary Stambuli (Kisagwa)

NAKUPENDA AHMADIYYA

1. Utukufu wa mbinguni, na ule wa ardhini.
Mmiliki ni Rabani, Mola rabbil ghalamin.
Aloniangaza dini, dini yake ya Manani.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

2. Muhammad lake jina, la pili umechukua,
Ahmadi ndio jina, kwake ulilolitwaa.
Kuongoza insana, ili wasije potea.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

3. Umetokea jangwani, barani uarabuni.
Kwa mafundisho ya dini, yaliyo jaa amani.
Ukashinda nafsi duni, Islam ikawa ndani.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

4. Elfu moja nne mia, miaka ilipofika.
Dunia alitujia, tulomngoja kufika.
Seyyidna Ahmadiyya, kujaeleza hakika.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

5. Rahmani limwambia, apande mbengu ya insa
Ahmadiyya ikanzia, moja nane nane tisa.
Na giza kuliondoa, dini ya kufwata visa.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

6. Mungu Mmoja twaomba, bila ya kushirikisha,
Uvivu hujatukumba, wa Mola kumdumisha.
Kwa sauti twajigamba, hata kitukufurisha.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

7. Quran kisha na Sunnah, hadithi zinafwatia.
Ndiyo tunavyojivuna, mwongozo wa kushikia.
Maneno ya kujashona, mbali twayatupilia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

8.Tunachopata hutoa, dini kuindeleza,
Mbinguni kujijengea, majengo ya kupendeza.
Kilicho bora achia, kwa Mungu Mola Muweza
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

9. Sala tano kila siku, kwa kudumu simamisha
Tahajudi za usiku, nazo kuziimarisha.
Tunaomba kwa shauku, Al Mujibu pitisha.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

10. Al Qayyum wa milele, pekee Atabakia.
Viumbe vyote vifile, nuruye itabakia.
Ni yule yule wa kale, Ametudhihirikia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

11. Kwa ishara kuonesha, kwetu si hutuletea.
Matetemeko hushusha, kwa wanaotukataa.
Kwetu sisi meepusha, balaa kutotutia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

12. Rahiim Hajatuacha , kila mtu kuamua.
Katuchagulia picha , Khalifa wa mfanoa.
Bila ya kushika ncha, amani kuhubiria.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

13. Kiongozi wa mfano, dunia kuionyesha.
Suluhu na maungano, dunia kuifundisha.
Kuondoa migongano, Islam yafundisha.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

14. Mapenzi yetu kwa wote, bila chuki kwa yeyote
Kauli mbiu ya wote, upendo pande zote.
Bila tazama chochote, kwa waabudu chochote.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

15. Twasema hayo kwa moyo, pia kwa kudhihirisha
Rehema iso na choyo, Islam ya fundisha.
Na huruma ya mioyo, daima tunadumisha.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

16. Nimejaribu tafuta, wala kasoro sioni.
Kwa ukweli wa kuvuta, uliojaa yakini.
Ya Mola kumtafuta, yajiweka hadharani.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

17. Mafunzo ya Qurani, hadharani kuyaweka.
Toka lile la mwanzoni, hadi la mwisho kushuka.
Nayo elimu ya ndani, kwa watu kuipeleka.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

18. Tayari kuweka kando, ya uzushi walotia.
Pia kufungua pindo, ya Manani kukazia.
Ni washetani upindo, akili kuiachia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

19. Kama sifa za kusifu, ni hii yaifalia.
Yaepuka upotofu, wa mambo kujitungia.
Ile ya zama nyoofu, imani twaifatia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

20. Nimejaribu kusema, machache yalonijia.
Naombeni kusimama, na kalamu kuachia.
Kwa uwezo wa Karima, kwa hapa lipofikia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

Masihi Omary Stambuli (Kisagwa)

UMOJA HAWANA

1. Hasa kanuni ya haki
Sehemu mbili haitaki
Yenyewe hasa hubaki
Sehemu iliyo moja

2. Sehemu inayopingana
Haki hatari haina
Na katu hutaiona
Kuwa hapo isitawi

3. Eti makundi Islamu
Yenye makundi uhasimu
Waweze kujiheshimu
Wawe wamoja wa dhati

4. Vipi wapate Khalifa
Watu wenye khitilafa
Na wao wengine kufa
Wengine huchekelea

5. Hilo haliwezekani
Nasema toka moyoni
Ni ndoto za mchanani
Ntibabara unaota

6. Ahmadiyya wamepinga
Sababu mewatinga
Si kuwa wamejiunga
Eti wanao umoja

Hassan Sango (Jang Muqaddas, kwenye karatasi)

AHSANTE SANA

Bismiullah naanza, mdogo naanzilia
Namshukuru Muweza, siha kunijaalia
Ni yeye alonitunza, shukuru kuwatolea
Kwa mengi nilojifunza, nalishukuru darasa

Nalishukuru darasa, kwa mengi nilojifunza
Sio kupika sambusa, elimu nazungumzia
Wapo walojitutusa, wote sitawapuuza
Kwa mengi walonifunza, nawashukuru walimu

Nawashukuru walimu, kwa mengi walonifunza
Muda yeye ni muhimu, Machombe alinikuza
Kwa mengi hasa magumu, ngangari walijikaza
Kwa mengi nilojifunza, nawashukuru wadau

Nawashukuru wadau, tumbo tumbo walipopuuza
Wao hawakudharau, elimu wakawekeza
Daima sitasahau, dua ninaiongeza
Ya Allah ya Muweza, Ghofiri yao madhambi

Zaid A. Machombe (Mdogo)
Mabibo, Dar es salaam

KUPAA NA KUTUA

Ni Roma pale mwanzoni, dini yake ilikua
Kusoma Kuruani, utatu kaachilia
Akakiri kwa imani, Khatam wa Manabia
Ni Muhamadi Bashiri, alo siraja Munira

Kasimama darasani, umombo kuwapatia
Ili wahubri dini, ufikaji wa Masia
Kwa hili Rabi Manani, sote tunaomba dua
Aipate busitani, maalimju B.K. Heri

Aling'ara gazetini, *Mapenzi ya Mung*u sikia
Makala zake makini, ni bingwa wa kuchambua
Hasa wale wapinzani, makovu kuwaachia
Kwa hilo Mola Kauma, twamuombea salama

Kaditama kituoni, sisi sote wa Jalia
Kama ndege wa angani, tunasubiri kutua
Tuo letu kaburini, gizani pasipo taa
Amali zako ni nuru, itayofukuza giza

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Bukoba, Uswahilini

DUNIA KOFI LA NYUMA

Dunia kofi la nyuma, Taharuki tunda lake
Moyo wangu wasimama, Wapi jiwe nieleke
Dunia yaenda kasi, Vinywa wazi yatuacha

Njaa miaka mitano, Chakula moja rakaa
Ndoani mifarakano, Dunia yashuhudia
Dunia yaenda kasi, Vinywa wazi yatuacha

Ghafla moto wa Moro, Nchi yawa simanzini
Mafuriko ya Mhoro, yatupeleka njaani
Dunia yaenda kasi, Vinywa wazi yatuacha

Wakubwa waanza vita, Waumiao ni sisi
Chuki imeshajikita, Vifuani mwa Unasi
Dunia yaenda kasi, Vinywa wazi yatuacha

Maisha yawa insta, Mitandao yawa dira
Twapost bila ya posta, umbea wawa ajira
Dunia yaenda kasi, Vinywa wazi yatuacha

Hili ni kofi la nyuma, Hugeuza utokako
Hukumbusha lengo mama, Kumuabudu Molako
Dunia yaenda kasi, Vinywa wazi yatuacha

Zama zataja Masihi, Njooni mumpokee
Ye ndo mokozi sahihi, Upako sio Korie
Dunia yaenda kasi, Vinywa wazi yatuacha

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721

Kijana na Mbwa Mwitu

Hapo mwanzo palikuwa na kijana mchungaji ambaye alichoshwa na kukaa kilimani akitazama kondoo wa kijiji. Kwa kujifurahisha akavuta pumzi kubwa na kupiga mayowe, "Mbwa mwitu! Mbwa mwitu! Mbwa mwitu anakimbiza kondoo hukuuu!"

Wanakijiji wakaja wakikimbilia kilimani kumsaidia kijana kumfukuzilia mbali mbwa mwitu. Lakini walipowasili kileleni, hawakukuta mbwa mwitu. Kijana akaucheka mwonekano wa nyuso zao zilizoghadhibika.

"Usiitie 'mbwa mwitu', we kijana mchungaji, wakati hakuna mbwa mwitu!" walimwambia wanakijiji. Walirejea chini ya kilima wakinung'unika.

Baadaye, kijana akaita tena, "Mbwa mwitu! Mbwa mwitu! Mbwa mwitu anakimbiza kondoo hukuuu!" Akifurahia utukutu wake, aliwatazama wanakijiji wakikimbilia kilimani kumsaidida kumfukuza mbwa mwitu.

Wanakijiji walipoona hakuna mbwa mwitu wakasema kwa ukali, "Toa mayowe yako ya woga panapokuwa na shida kweli! Usiitie 'mbwa mwitu' wakati HAKUNA mbwa mwitu!"

Kijana akakenua tu na kuwatazama wakirejea tena chini ya kilima huku wakilalamika.



Baadaye, aliona mbwa mwitu WA KWELI akinyemelea kondoo wake. Akiwa ametahamaki, alichopoka huku akiita kwa sauti kadiri alivyoweza, "Mbwa mwitu! Mbwa mwitu!"

Lakini wanakijiji wakafikiria alikuwa anajaribu kuwapumbaza tena, na kwa hiyo hawakuja kusaidia.

Jua lilipozama, kila mtu alikuwa anashangaa kwa nini kijana mchungaji hajarejea kijijini na kondoo wake. Wakaenda kilimani kumtafuta kijana. Wakamkuta akilia.

"Kulikuwa na mbwa mwitu kweli hapa! Kondoo wametawanyika! Nimeitia, "Mbwa mwitu!" Kwa nini hamkuja?"

Mzee mmoja alijaribu kumliwaza kijana wakati wanakijiji walivyokuwa wakirejea kijijini.

"Tutakusaidia kuwatafuta kondoo waliopotea asubuhi," alisema mzee, huku akiweka mkono wake kumzunguka kijana, "Hakuna mtu anayemwamini mwongo... hata anapokuwa akisema ukweli!"

• •

Hadithi hii inatufundisha nini?

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno kwa kuyazungushia na Penseli

W	A	T	H	A	M	U	D	I	J	M	I	Z	T	I	R	Q	N	Q	Y
L	G	D	W	G	P	I	F	K	A	B	F	B	V	M	S	L	M	Q	X
T	T	L	T	R	T	G	U	W	M	W	T	B	R	I	F	L	K	M	K
D	R	M	K	I	X	F	I	A	M	V	B	T	H	P	T	H	A	R	J
K	L	B	K	L	I	L	H	O	C	H	R	H	P	K	E	E	K	M	R
T	R	I	Y	L	U	D	I	M	A	N	A	B	I	I	U	N	N	J	N
W	S	J	I	Y	W	N	B	Q	U	I	J	R	V	V	B	M	D	D	Z
M	X	D	N	N	I	C	H	G	H	S	X	N	Z	M	A	W	D	A	O
R	A	A	V	M	L	N	N	A	G	M	T	V	P	U	D	O	B	T	M
S	Y	P	A	M	P	I	R	Z	L	A	W	F	M	H	H	N	D	M	S
N	A	A	L	T	B	A	T	C	X	I	K	H	D	A	I	G	V	P	H
Y	W	H	W	M	J	M	H	M	T	L	M	K	U	M	R	O	L	Q	U
R	N	W	A	A	W	K	P	A	W	X	C	Q	Z	M	I	Z	N	A	K
L	C	M	H	B	F	V	B	R	J	U	R	P	U	A	F	O	M	X	U
L	M	S	Y	W	A	W	V	D	B	I	J	L	R	D	U	I	K	B	R
B	I	N	A	D	A	M	U	M	Z	N	R	I	I	P	T	H	Y	Y	A
K	H	I	F	A	D	H	I	T	D	T	L	A	Z	A	Y	Y	X	W	N
V	J	T	Z	H	V	U	K	R	I	S	T	O	Y	A	N	D	F	J	I
V	H	K	H	A	T	A	M	A	N	N	A	B	I	Y	Y	I	N	V	F
H	H	P	V	Y	N	G	K	M	S	A	M	A	H	A	T	C	G	N	N

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jinsi ya Kupika Keki ya Nyama

Na **Mubarakati S. Mbaruk Kapilima**



Maandalizi

Nyama robo 1/4
Unga nusu ½
Siagi ½ (Prestige)
Chumvi kidogo sana
Mayai 16
Hoho kubwa 1
Karoti mbili 2
Kitunguu thaumu kidogo
Pilipili manga ya unga
Baking powder kijiko kimoja cha chai kisijae

Jinsi ya kuipika

Chukua nyama yako iliyosagwa uweke chumvi kidogo na kitunguu thaumu na pilipili manga yako ya unga, iweke jikoni mpaka iive na ikauke. Kumbuka ukiichemsha haiwekwi maji.

Chukua siagi yako weka kwenye bakuli ipige na mashine au mwiko hadi iwe rojo, waweza ongeza chumvi kama siagi unayotumia itakuwa haina chumvi ya kutokeza. Ila vizuri utumie prestige kwa sababu utakwepa kuweka chumvi, kisha weka mayai kumi na mbili uchanganye na baking powder na kuweka ndani ya mchanganyiko wetu. Ukishakamilika paka trei au chombo chako cha kuokea siagi na uumimine mchanganyiko wako kama keki kwenye chombo chako hicho.

Baada ya hapo unachukua nyama unaimwaga juu yake, unakata hoho kwa kufuata muundo wake wa duara, kisha unaisaga karoti katika kibati cha kusagia kisha kwa pamoja unavitawanya juu ya ulee mchanganyiko.

Mwisho unachukua mayai manne yaliyobaki unayapiga sana kwenye bakuli kisha unamwagia juu yake. Unaoka kwa moto wa wastani kama wa keki. Na ikishaiva unaacha ipoe ndio unaitoa na kuikata.

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Je Mungu Ana Rangi?

Na **Musa Salum Mgeleka**

(Jipakeni) Rangi ya Allah: na ni nani aliye mbora wa Rangi kuliko Allah? Na ni Yeye tu Ndiye tunamwabudu. (Surah 2:139)

Neno SIBGH, "RANGI," mradi wake ni
1◎ Dini;
2◎ Kanuni za sheria; 3◎Tabia ambayo Mwenyezi Mungu amempa mtu;
4◎ Ubatizo (Akrab).

Dini inaitwa SIBGHA kwa sababu inamwenea mtu kama rangi. Hivyo SIBGHATALLAHI maana yake ni "shika au fuata dini ambayo Mwenyezi Mungu anakutaka uishike au uifuate."
Huo ndio hasa ubatizo wa kweli unaoweza kumfanya mtu aige sifa za Mwenyezi Mungu.
Ubatizo huu ni Mtukufu na mbali kabisa na ubatizo wa Kikristo ambao unatafuta kumpatia mtu kusamehewa dhambi zake, na kumpatia mtu uhai wa milele, kwa tendo dogo la kumchovya ndani ya maji au kumnyunyuziayo wakati wa kumtia Ukristo.
Dini ya Mwenyezi Mungu haina maana kwamba Mwenyezi Mungu anafuata dini yo yote ile. Ina maana tu kwamba ni ile dini iliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu.
Dini ndio Inakanuni na Sheria za Allah na Dini ndio Inambatiza Mtu kukamata Sheria na Kanuni za Allah.
Sifa hii ya Rangi ni Sifa Mahusu kwa Vitu ili Vionekane, Vitoe Mwanga, Viakisi, Mvuto n.k Rangi hutumika kwenye Vitu.
Rangi ipi Allah Ameikusudia, Anajibu mwenyewe
Bila shaka dini hasa mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu; na waliopewa Kitabu hawakuhitilafiana ila baada ya kuwajia elimu, kwa sababu ya uasi uliokuwa kati yao; na anayezikataa Aya za Mwenyezi Mungu, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhesabu. (Surah 3:20)
DINI ni Utii wa Mungu, Kujinyenyekea kwa Mungu, Sheria anazotumia Mungu Kutawala, Sheria zilizo Kamilika, n.k
Mungu watu wote wanajua Amekamilika hivyo Dini nayo yapaswa Kuwa imekamilika kwa Misingi yake na Yenyewe Ijitangaze kuwa Imekamilika na Kikubwa Kidhahiri Ionyeshe Imekamilika.
Rangi hii Itaonekana na Kuenea kana kwa Dhilisho lake Mungu.
Allah Ajaalie kutufanya sisi wanadamu kujipaka rangi Yake ili kusudio Lake litimie. Amin

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA

Kuomba Dua Ndani ya Sala

"Inapaswa kuomba dua ndani ya sala kwa lugha yako, kwani ari kamili hupatikana kwa sababu ya kuomba dua kwa lugha yako. Sura Fatiha ni neno la Mwenyezi Mungu nayo inatakiwa kusomwa kama ilivyo kwa lugha ya Kiarabu na sehemu ya Kurani Tukufu ambayo husomwa baada yake pia inatakiwa kusomwa kwa lugha ya Kiarabu. Baada yake yapaswa pia kusoma maombi mengine na Tahmiid kwa Kiarabu lakini inatakiwa kuelewa tafsiri yake. Pamoja na hayo, inapaswa kuomba dua kwa lugha yako ili utulivu wa moyo upatikane; kwani sala isiyokuwa na utulivu wa moyo si sala halisi. Siku hizi ni kawaida ya watu kusali kwa kusujudu haraka haraka kana kwamba ni kodi iliyotozwa na kisha huanza kuomba maombi kwa muda mrefu. Hii ni bidaa. Jambo hili la kufanya dua baada ya kutoa salamu katika sala halijagusiwa katu ndani ya hadithi za Mtume (saw). Watu wajinga huichukulia sala kama kodi na kuitenga na dua. Sala yenyewe ni dua. Kwa ajili ya shida zote za kidini au za kidunia na wakati wa kila taabu mwanadamu hupaswa kuomba dua ndani ya sala.

Dua hutakiwa kuombwa katika kila hatua ndani ya sala. Ombeni dua nyingi katika Rukuu, baada ya kusoma Tasbiih, katika sujuda, baada ya sujuda, baada ya kusoma Tashahhud, mkiwa mmesimama na baada ya Rukuu ili mpate kunufaika sana. Yapaswa moyo utiririke katika dua (kwa unyenyekevu) kama yatiririkavyo maji. Dua ya namna hii hutakasa moyo. Ikiwa dua hii inapatikana mtu anaweza kudumu katika sala kutwa nzima. Dua zinatakiwa kuombwa kwa Allah subhana wataala ili kuepukana na kukamatwa na dhambi.

Dua ni tiba ambayo kwayo sumu ya dhambi huondolewa. Baadhi ya wajinga hudhani kuwa sala inavunjika kutokana na kuomba dua kwa lugha yako. Mtazamo huu si sahihi. Sala ya watu kama hawa yenyewe imesheharibiwa tayari."

(Malfuzat, Juz. 9, uk. 54,55, toleo jipya)



Maadhimisho ya Mwana Aliyeahidiwa Jamia Ahmadiyya



Amir Jamaat akitoa zawadi kwa mwanafunzi bora wa shule ya msingi Ahmadiyya



Wanafunzi na uongozi wa shule ya msingi Ahmadiyya katika picha ya pamoja na Amir Jamaat wakati wa mahafali



Khuddam wa Pwani baada ya Kambi ya Malezi iliyofanyika Kibiti



Rais na Sheikh wa mkoa wa Dar es salaam wakiwa katika ziara ya matawi



Wanajamaat wa Kagenyi wakikarabati nyumba ya mwanajumuiya iliyoezuliwa na upepo



Wanajamaat wa Njinjo waliopatwa na maafa ya mafuriko wakipokea msaada



Washiriki wa Maadhimisho ya Siku ya Mwana Aliyeahidiwa mkoa wa Dodoma



Maadhimisho ya siku ya Mwana Aliyeahidiwa kanda ya Kitunda



Wanajamaat wa Kitonga wakifanya Wakal Amal katika maeneo ya Jamaat

Upendo na Utii wa Masahaba kwa Mtume saw

Kutoka toleo Lililopita

Baada ya hapo, siku fulani, mshairi fulani maarufu wa kiarabu aliyeitwa Labid, alikuwa ameketi miongoni mwa wakuu fulani wa Makka akiwasomea mashairi yake na akasoma ubeti mmoja uliosomeka Wa kullu na'iimin laa mahaalata zaailun uliokuwa na maana ya; Hatimae kila neema ni yenye kufutika. Uthman ra akasema: si sahihi, neema za Peponi ni za kudumu milele.

Labid alikuwa ni mtu mkubwa sana aliyeheshimika. Aliposikia jibu hilo, akapandwa na hamaki na kusema: "Enyi watu wa Quraish! Hapo kabla mgeni wenu hakuweza kudhalilishwa namna hii, sasa hii desturi mpya imeanza lini?" Hapo mtu mmoja akasema; huyu ni mtu mmoja mpumbavu, usiyajali maneno yake. Hadhrat Uthman ra akaendelea kuyasisitiza maneno yake na kusema kuna jambo gani la upumbavu? Nilichosema ni kweli. Hapo mtu fulani akasimama na kumpiga ngumi ya nguvu sana usoni iliyosababisha jicho lake kuvimba.

Wakati huo Waliid alikuwa ameketi katika kikao hicho. Kulikuwa na urafiki mkubwa kati yake na baba ya Uthman. Alihuzunishwa sana kuiona hali ile ya mtoto wa marehemu rafiki yake. Lakini kulingana na desturi za Makka, kwa kuwa Uthman hakuwa tena chini ya hifadhi yake, hivyo hakuweza hata kumhami. Kwa kuwa hakuweza kufanya lolote, hivyo akamwambia Uthman kwa uchungu: Ewe mwana wa ndugu yangu! Kwa haki ya Allah jicho lako hili lingeweza kusalimika na balaa hili wakati ulipokuwa ndani ya hifadhi madhubuti (yaani ulipokuwa ndani ya hifadhi yangu), lakini wewe mwenyewe uliiacha hifadhi hiyo na hatimae kuiona siku hii.

Uthman akajibu: "Hicho kimechonikuta nilikitamani mwenyewe. Wewe walihuzunikia jicho langu hili limepofuka! wakati jicho langu lililo zima lina hamu kubwa kwamba kwa nini halinitokei lililomtokea mwenzangu? Mfano wa Muhammad saw, Mtume wa Mungu, unatosha kwa ajili yangu, kama yeye anapata usumbufu, kwa nini mimi nisisumbuke? Ulinzi wa Allah unatosha kwa ajili yangu."

Mwandishi fulani akiielezea hali ya Masahaba wa Mtume saw anasema:

"Wale Waislamu wachache waliobakia Makka kwa kutohamia Uhabeshi, wao ndani kwa ndani walikuwa wakiwahubiria ndugu na jamaa zao, majirani zao, marafiki zao na wenzao. Mioyo ya baadhi yao ilikuwa ikipata nuru ya imani na wakawa wakijidhihirisha kwa kutangaza dini yao na wakawa wakishiriki na ndugu zao katika kupata vipigo na masumbufu. Lakini ni wachache mno walioiona nuru na halafu kutopata uwezo wa kutoikubali. Wao walikuwa wakiisubiri siku ile ambapo ufalme wa Allah utakapokuja duniani nao wapate kuingia humo.

Hadhrat Khubaib ra alishikwa mateka na jeshi la Musailimah Kadhaab baada ya kifo cha Mtume saw, basi Musailimah alimuitisha na kumuuliza kwamba: 'je wewe washuhudia kuwa Muhammad saw ni Mtume wa Allah?' Khubaib akasema; 'Naam.' Kisha Musailimah akamuuliza; 'Je unashuhudia kuwa mimi ni Mtume wa Allah?' Khubaib akasema: 'Hapana.' Hapo Musailimah akaamuru kwamba mkono mmoja wa Khubaib ra ukatwe na ukakatwa.

Kisha Musailimah akamuuliza tena: 'je unashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah?' Khubaib akasema: 'ndio.' Kisha akamuuliza tena: 'je unashuhudia kuwa mimi ni Mtume wa Allah?' Khubaib akasema; 'Hapana.' Hapo akaamuru Khubaib ra akatwe kiungo chake kingine cha mwili. Na kila baada ya kumkata kiungo cha mwili alikuwa akimuuliza kwamba je unashuhudia kuwa mimi ni mtume wa Allah na Khubaib alikuwa akijibu; Hapana. Kwa namna hii viungo vyake vyote vya mwili vikakatwa. Na hatimaye, akakatwa vipande vipande. Kwa njia hii, aliithibitisha imani yake na kuiaga dunia.

Abbas ra aliyekuwa baba mdogo wa Mtume saw aliyekuwa bado hajasilimu wakati huo, aliwaendea watu fulani wa Madina waliokuwa wamejumuika na Mtume saw kwa siri katika eneo fulani la huko Makka, wakiwa wamebeba dhimma ya kumkaribisha Mtume saw kuhamia Madina na kuwaambia:

"Enyi watu wa kabila la Khazraj! Kipenzi changu huyu (Muhammad saw) ni mtu mwenye kuheshimika ndani ya kaumu yake. Watu wa kaumu yake humlinda, wawe Waislamu au la. Lakini sasa yeye ameamua kuja kwenu. Enyi watu wa Khazraj! Kama yeye akija kwenu, basi Bara Arabu yote itakuwa dhidi yenu. Kama mwataka kumchukua huku mkilifahamu jukumu lenu na kuzielewa hatari zile zitakazokujieni kutokana na kuihami dini yake, basi mchukueni kwa furaha, waila jiepusheni na dhamira hii."

Kiongozi wa msafara ule alikuwa ni Al Barraa ra Alisema:

"Tumeyasikia maneno yako. Sisi tuko imara ndani ya dhamira yetu. Tumeyatoa mhanga maisha yetu kwa Nabii wa Allah. Sasa uamuzi ni wake. Sisi tutaukubali kila uamuzi wake.'

Hapo Mtume saw akaanza kuwapa mafundisho ya Islam na akawapa mawaidha ya Umoja wa Allah na kuwaambia kwamba kama wao wanatoa ahadi ya kuilinda Islam kama wawalindavyo wake na watoto wao, basi yuko tayari kwenda nao. Alikuwa hajamaliza kuongea maneno yake ambapo watu sabini na mbili wa Madina, kwa kauli moja, wakaitikia ndio ndio. Walipandwa na jazba wakati huo kiasi ya kughafilika na utukutu wa watu wa Makka na sauti zao zikavuma angani.

Abbas akawatahadharisha akiwaambia kelelen, kelelen. Isije watu wa Makka wakalifahamu tukio hili. Lakini wakati huo walikuwa wameshaipata imani. Sasa mauti kwao ilikuwa imeshakuwa ni jambo duni tu. Kiongozi wao mmoja alisema baada ya kusikia neno la Abbas ra:

"Ewe Mtume wa Allah! sisi hatuogopi. Wewe toa tu ruhusa sasa hivi tupigane vita na watu wa Makka tukiwa tayari kulipa kisasi cha dhulma waliyokutendea."

Mtume saw akasema; "Allah Hajanipa bado hukumu ya kusimama na kukabiliana nao." Baada ya hapo watu (hao) wa Madina wakafanya Baiat yake na kikao hicho kikaishia hapo.

Mtume saw alipokuwa akihamia Madina, walianza safari yao akiambatana na Hadhrat Abu Bakar ra wakiwa wamejificha ndani ya pango la Thaur, wakiwakwepa Maqureishi waliokuwa wakimsaka Mtume Muhammad saw kwa juhudi zote ili wamkamate na kumuua. Maqureishi wakakusanya jeshi fulani na kuanza kumsaka Mtume Muhammad saw Wakamchukua pia mtaalamu fulani wa kufuatilia nyayo ambaye, kwa kuzifuata alama za nyayo zao, wakafika hadi kwenye mlima wa Thaur. Baada ya kufika kule kwenye pango alikokuwa (Mtume saw) amejificha pamoja na Abu Bakar ra, (mtaalamu) yule akasema kwa yakini kabisa kwamba aidha Muhammad saw yumo ndani ya pango hili au atakuwa amepaa mbinguni. Wakati huo mlango wa pango ukiwa umezibwa na utando wa buibui na njiwa akiwa ametaga mayai yake juu ya utando huo.

Moyo wa Abu Bakar ra ulipoyasikia maneno yake haya ukashikwa na hofu kubwa na akaanza kumwambia Mtume saw kwa sauti ya chini kwamba: 'Adui ameshakaribia kabisa na sasa wakati wowote ule ataingia pangoni. (Mtume saw) akamwambia: Laa tahzan Inna Laaha ma'anaa: yaani usihofu ewe Abu Bakar, Mungu Yu pamoja nasi.

Abu Bakar ra akasema: Ewe Mtume wa Allah! Mimi siihofii nafsi yangu, kwani mimi ni mtu tu wa kawaida, nikifa itakuwa ni mtu mmoja tu amekufa. Ewe Mtume wa Allah, hofu yangu ilikuwa hii tu kwamba kama uhai wako upate shida yoyote ile, basi jina la dini na utawa vitatoweka duniani. (Mtume saw) akasema: "usijali, hapa hatuko wawili, bali wa tatu wetu Yuko pia Allah."

Nako Madina habari zikawa zimeshaenea kwamba Mtume saw ameshaondoka Makka na hajulikani aliko na zawadi kubwa imetangazwa kwa atakayemrejesha Muhammad saw huko Makka akiwa hai au amekufa. Ikawabainikia watu wa Madina kuwa bila shaka Mtume saw yu njiani kuja Madina.

Watu wa Madina wakawa wakimsubiri tangu siku ile. Kila siku misafara yao ilikuwa ikitoka nje ya Madina kwa maili kadhaa kwenda kumtafuta na jioni walikuwa wakirejea wakiwa wamekata tamaa.

Myahudi fulani alikuwa wa kwanza kuwaona ngamia wa Mtume saw huko Quba walipokuwa wameweka kituo kwa muda. Myahudi huyo alipanda juu ya kilima na kuwatangazia kwa sauti ya juu watu wa Madina akiwaambia:

"Enyi wana wa Qaila! yule mliyekuwa mkimsubiri amekuja."

Baada ya kusikika kwa sauti hii, kila mtu wa Madina alitoka mbio kuelekea Quba. Wenyeji wa Quba walifurahi kupindukia baada ya kufahamu kwamba Nabii wa Allah sasa anakuja kuishi pamoja nao. Shangwe, vifijo na nderemo zilisambaa katika anga za Madina na huku akina mama wakipiga dufu na kuimba Qaswida maarufu ya kumkaribisha Mtume saw isemayo:

طلع البدر علينا من ثنيات الوداع
وجب الشكر علينا ما دعا لله داع
أيها المبعوث فينا جئت بالامر المطاع

"Mwezi mpevu wa usiku wa tarehe 14 umetuangazia katika eneo hili la Widaa, na kadiri atakavyokuwepo duniani yule aitaye kwa Allah, basi ni wajibu wetu kuishukuru hisani hii. Na ewe yule ambaye Allah Amekutuma kwetu, hukumu yako itatiiwa kikamilifu."

Mtume saw alipoingia Madina kila mtu alikuwa anataka kwamba Mtume saw afikie nyumbani kwake. Katika mitaa ile aliyokuwa ngamia wake akipita, watu wa familia mbali mbali za mitaa hiyo walikuwa wametoka nje ya nyumba zao, wakimkaribisha Mtume saw na huku wakisema: Ewe Mtume wa Allah, hii ni nyumba yetu na hii ndio mali yetu na hizi ni nafsi zetu zilizo tayari kukuhudumia. Ewe Mtume wa Allah! Sisi tunao uwezo wa kukulinda, hivyo ishi ndani ya nyumba yetu.

Watu wengine walikuwa wakisonga mbele kwa jazba na kuzikamata hatamu za ngamia wake ili wamteremshe nyumbani kwao. Lakini yeye alikuwa akitoa jibu hili hili kwa kila mtu kwamba:

"Muacheni ngamia wangu, kwani leo anaelekezwa na Allah. Atasimama pale pale atakapopapenda Allah."

Hatimae ngamia yule akasimama kwenye kona fulani ya Madina iliyo kwenye ardhi ya mayatima wa Banu Najar. Akasema kwamba yaonekana kuwa matashi ya Allah ni haya kwamba sisi tuishi hapa.

Baada ya hapo Mtume saw akauliza: "Ni nyumba ya nani iliyopo karibu zaidi." Abu Ayub Ansari akajitokeza na kusema: Ewe Mtume wa Allah! Nyumba yangu ndio iliyo karibu zaidi nayo iko kwa ajili ya kukuhudumia. (Mtume saw) akamwambia: "Nenda nyumbani ututayarishie chumba kimoja."

Nyumba ya Abu Ayyub ilikuwa ni ya ghorofa mbili. yeye akapendekeza kwamba Mtume saw akae kwenye ghorofa ya juu. lakini Mtume saw akapendelea sehemu ya chini kutokana na wazo hili kwamba watu watakaokuwa wakija kumtembelea wasisumbuke.

Mtume saw aliposisitiza, basi Hadhrat Ayyub Answar ra akakubali kwa shingo upande akisema: "sawa wewe ishi katika sehemu ya chini ya nyumba."

Matokeo yakawa hivi kwamba usiku mzima mume na mke walikosa kabisa usingizi kwa mawazo haya kwamba Mtume wa Allah saw analala chini yao, sasa wao wawezeje kuwa wenye kuhusika na utovu huu wa adabu kwamba wao walale kwenye ghorofa ya juu.

Ikatokea pia kwamba chombo fulani cha kuhifadhia maji kikaanguka wakati wa usiku, akichelea kwamba isije maji yakavujia huko chini alikolala Mtume saw, Hadhrat Ayyub ra akaharakisha kuiweka shuka yake juu ya maji yale yaliyomwagika na kuyakausha mara moja.

Alfajiri akawasili tena kwa Mtume saw na kumweleza habari zote ambapo Mtume saw akakubali kwenda kuishi sehemu ya juu.

Kila siku Hadhrat Ayyub ra alikuwa akitayarisha chakula na kumpelekea Mtume saw Na nyumba nzima wakawa wakisubiri na kula furaha ya makombo yaliyokuwa yakibakia.

Baada ya siku kadhaa, wenyeji wengine wa Madina pia wakasisitiza wakiomba nao wapate fursa ya kumhudumia mgeni huyo wa baraka. Waislamu wa Madina wakawa wanamletea kwa zamu chakula nyumbani kwake hadi nyumba ya Mtume saw ilipokuwa tayari.

Siku moja, mjane fulani wa Madina alikuja kwa Mtume saw akiwa ameandamana na mtoto wake wa pekee aliyekuwa na umri wa miaka tisa au minane hivi. Akamuomba kwa unyenyekevu kwamba Mtume saw ampokee mtoto yule ili awe mtumishi wake. Mtume saw akampokea mtoto huyo na akawa mtumishi wake hadi mwisho wa uhai wake Mtume saw Mtoto huyo alikuwa ndiye Hadhrat Anas ra aliyekuja baadae kuwa mwanazuoni mkubwa mwenye kumiliki utajiri mkubwa na kupata pia baraka ya umri mrefu wa zaidi ya karne moja.

Itaendelea toleo Lijalo

Mwana Aliyeahidiwa as

Inatoka uk 12

na kizazi chako. Kijana mzuri na mtakatifu atakuja kama mgeni wako. Jina lake ni Imanueli na Bashir. Amejazwa roho takatifu, na ameepukana na uchafu wote. Ni nuru ya Allah. Amebarikiwa yule ajaye kutoka mbinguni. Atafuatana na rehema ambayo itawasili pamoja naye. Atahusishwa na utukufu, ukuu na utajiri. Atakuja duniani na atawaponya wengi wenye maradhi kwa njia ya sifa zake za Umasihi na kwa njia ya Baraka za Roho ya kweli. Yeye ni Neno la Allah kwani ukarimu na heshima ya Allah imemtuma na Neno la Utukufu. Atakuwa na akili sana mno na ufahamu na atakuwa mpole wa moyo na atajazwa elimu ya nje na ndani. Atawafanya watatu kuwa wanne (hii maana yake haikubainishwa). Ni Jumatatu, Jumatatu iliyobarikiwa. Mwana wa kiume, furaha ya moyo, aliyenyanyuliwa, mtukufu, mdhihirishaji wa Aliye ni wa Mwanzo na Mwisho, alama ya Yule Aliye Mkweli na wa Juu; kama kwamba Allah Ameshuka kutoka mbinguni. Kufika kwake kutabarikiwa sana sana na atakuwa sababu ya kudhihirika kwa Jalali ya Uungu.

Nuru inakuja, nuru hasa, nuru iliyosingwa na Allah uturi wa mapenzi Yake. Tutampulizia roho yetu atahifadhiwa chini ya Kivuli cha Mwenyezi Mungu. Atakuwa upesi upesi katika umbo na atakuwa sababu ya kukombolewa wale waliomo utumwani. Atajulikana mpaka pembe za dunia na mataifa yatabarikiwa kwa ajili yake. Ndipo atachukuliwa juu mbinguni kwenda mahali alipotayarishiwa na jambo hili limekwisha katwa" (Tangazo la tarehe 20 Februari, 1986).

Baada ya maelezo ya utabiri Hadharat Khalifatul Masihi V atbt akanukuu maelezo ya Hadhrat Muslih Maud ra kuhusu Masihi Aliyeahidiwa as alivyoomba kwa unyenyekevu mkubwa kwa kujitenga peke yake katika sehemu maalum na jinsi kwa shani kubwa maombi haya yalivyokubaliwa na Allah.

Hadhrat Muslih Maud ra anasema miaka 58 toka siku ilipotangazwa bishara hii mnamo tarehe 20 Februari 1886 katika mji huu wa Hoshiyar-pur katika nyumba ile (na Mwana Aliyeahidiwa ra akanyoosha kidole chake kuelekea kwenye nyumba iliyokuwa mbele yake ambamo Masihi Aliyeahidiwa as aliomba dua hii).

Hadhart Muslih Maud ra anasema katika nyumba ile Masihi Aliyeahidiwa as aliomba dua mbele ya Allah kwa siku 40 mfululizo na Allah akampatia ishara na kwamba sio tu ile ishara itatimia kwa kukubaliwa dua zake bali atapewa mtoto mwenye sifa maalum atakaejaaliwa elimu ya nje na ndani itakayo kuwa msaada mkubwa katika kuihami na kuihudumia dini ya Kiisalam.

Khalifa mtukufu atba anasema nchi yoyote ambayo imejaaliwa Jamaat kuingia, katika Jamaat ile Mwana Aliyeahidiwa amekuwa mashuhuri na maarufu.

Hadharat Muslih Maud ra anasema kwamba lilipotolewa tangazo hili wapinzani walipiga kelele kupinga kwamba kuja kwa mtoto huyu kuna ajabu na tofauti gani, kwani watoto huzaliwa kwa watu wengine kila siku.

Masihi Aliyehidiwa as tarehe 22 Machi 1886 akatoa tangazo ambamo alitoa jibu lake kwa kusema kuwa hii haikuwa bishara ya kuja kwa mtoto tu wa kawaida bali kama ishara ya ukweli wa mtume saw, mtoto huyu atakaye kuja atakuwa mwenye baraka nyingi za kimwili na kiroho nazo zitaenea katika dunia nzima.

Baadhi ya wapinzani wanapinga kwamba mwana huyu atakuja baada ya karne 3 au 4.

Katika kujibu hili Hadhrat Muslih Maud ra anasema jambo hili linawezekana namna gani?

Wapinzani wa dini ya Islam wanataka ishara ya ukweli wake sasa na wao wanasema ishara hiyo itakuja baada ya karne nne baadae. Hili ni jawabu gani na ni yule mtu aliye mjinga wa mwisho tu anayeweza kulitoa jawabu kama hili.

Yaani maana yake bishara hii kutimia kwake kuna takiwa kutokea muda huu huu ambapo wale walioomba bado wako hai na wanaweza kuiona, si baada ya karne 3 au 4.

Hadhart Muslih Maud ra akielezea makusudio na malengo ya bishara hii, anasema:

1. Wale wanaotamani kupata uhai wa kiroho waweze kuhuishwa
2. Na wale ambao waliozikwa makaburuni waweze kufufuliwa
3. Na ili iweze kudhihirika shani na utukufu wa dini ya Islam na ubora wa maneno ya Allah ufahamike kwa watu.
4. Ili ukweli uweze kudhihirika na baraka zake na batili iondoke na nuksi zake.
5. Ili watu waweze kufahamu kuwa mimi ni Allah nafanya nitakalo.
6. Ili wawe na yakini kuwa mimi niko pamoja nawe.
7. Na ili wale wasio mwamini Allah ishara iwe wazi kwao.
8. Na ili njia ya waongo iwe wazi.

Na yale yaliyo katika bishara hii yanahitajika kutimia sasa na wala sio hapo baadae ambapo wala si wale walioiomba watakuwa hai, wala si watoto wao na wala si vizazi vyao.

Hadhrat Musleh Maud ra anasema kwamba mimi naapa kwa jina la Allah yule mtoto Aliyeahidiwa katika bishara hii ni mimi, nayo imetimia katika dhati yangu, na imekuwa hoja iliyo hai kwa maadui wa dini ya Islam.

Hadhart Musleh Maud ra anaendelea kusema kuwa nani anaweza kuwa na nguvu ya kumleta mtoto ambaye atakuwa maarufu na anayejulikana katika pembe zote za dunia kama si Allah.

Na yeye (Allah) Akaifanya kutimia bishara hii katika dhati ya mtoto huyu ambaye kuhusiana naye madaktari walisema kuwa sijui ataendelea kuwa hai au hataendelea kuwa hai.

Pia Allah Akamjaalia elimu nyingi kwa njia ya malaika ambapo hapo mwanzo alikuwa hana sifa yoyote ya usomi, na akampa elimu ya Qurani tukufu.

Hadhart Muslih Maud ra akaendelea kusema kuwa kama kuna mtu yeyote anayedai kupata elimu kubwa kutoka kwa Allah aje kwenye mashindano na mimi, kwani katika zama za leo hakuna mtu yeyote aliyejaaliwa elimu ya Qurani tukufu zaidi yangu mimi. Na Allah Amenisimamisha ili kuzibatilisha dini zote za uongo, nami naapa kwa jina la Allah kuwa wote washindwa mbele yangu na kwamba jamaa zao zote na mipango yao yote itaangamia.

Khalifa mtukufu atba anasema tangazo hili halikuwa la mchezo bali lilikuwa ni tangazo kubwa na katika zama zake za Ukhalifa kila siku katika muda wote kwa miaka 52 lilishuhudiwa likitimia siku hadi siku.

Hadhart Muslih Maud ra anasema mimi sifanyi fakhari juu ya heshima yangu hii, bali mimi naonesha ukweli wa bishara hii ya Allah mbele ya dunia, haya ni mapenzi ya Allah na ukweli huu hautakoma kutimia mpaka wote ukamilike na ili Islam iweze kuenea dunia nzima, na Ukristo ushindwe, na hakuna yeyote atakayeuokoa Ukristo kutokana na kushindwa kwake, na kushindwa kwa dini ya Kikristo kutatokea katika uhai wangu au katika uhai wa wafuasi wangu nayo itanyauka kama ua.

Hadhrat Musleh Maud ra anasema kuwa bishara hii tayari imekwishatimia katika dhati yangu sasa hivi mimi nawatangazia wale waliokuwa wafuasi wangu majukumu yanayopaswa kutekelezwa na wao. Kwa sababu wao ni wasadikishaji wa kwanza wa bishara hii kwamba wanatakiwa kuleta mabadaliko ya kweli katika maisha yao na kukubali kumwaga damu zao mpaka tone lao la mwisho kwa ajili ya mafanikio na ushindi wa dini ya Islam.

Hadhart Muslih Maud ra anasema, imesemwa na Hadhart Masihi Aliyeahidiwa as kuwa ninyi mfurahi na mruke ruke kwa sababu ya nuru itakayo kuja pamoja na bishara hii. Mimi siwazuieni kufurahia bali mimi nawakumbusheni kuhusu majukumu yenu kuwa ninyi msiyasahau.

Imesemwa pia katika bishara kuwa mtoto huyo atakuwa upesi upesi, kwa mnasaba huo ninyi pia mnahitajika kuacha uvivu na uzembe. Allah amsamehe yule ambaye anabaki nyuma kama wanafiki badala ya kusonga mbele. Kwa hiyo ninyi mnatakiwa kutembea sambamba nami kwani mbingu na dunia vinaweza kutoweka lakini maneno ya Allah hayataacha kutimia mpaka yote yatimie.

Khalifa mtukufu Vatba anasema kwamba Allah Ataujaalie nguvu ya kuendelea kufanya kazi, wala tusiwe watu wenye kushabikia sherehe tu bali sisi tuendeleze mbele kazi ile ambayo kwayo Allah alimtuma Masihi Aliyeahidiwa as.

Khalifa mtukufu atba anasema sasa nitaeleza kwa kifupi kazi kubwa mbalimbali alizozifanya Mwana Aliyeahidiwa ra. Katika bishara imesemwa kuwa yeye atajaaliwa elimu ya ndani na nje. Maelezo yake kwa kifupi ni kama ifuatavyo: Kitabu ambacho ni mjumuiko wa hutuba mbalimbali pamoja na vitabu alivyoandika na majarida yake vimeshachapwa, jina lake ni Anwarul Ulum, jalada zake 26 zimekwishachapwa.

Vilevile kuna kitabu kingine kinachoitwa Khutubat-e-Mahmood (mkusanyiko wa hutuba za Ijumaa) kina jalada 39.

Kitabu kingine ni Tafsir-e-saghiir (Tafsir ya Qurani katika lugha ya Kiurdu yenye malezo mafupi) yenye kurasa 1071.

Na kitabu cha Tafsir-e-kabiir chenye majalada 10, kurasa 5907 namo kuna sura 59 zimefasiriwa na kutolewa maelezo marefu ya kina.

Kuna darasa mbalimbali za Qurani alizozitoa katika nyakati mbalimbali kurasa zake zinafikia 3095.

Khalifa mtukufu Vatba anasema maelezo kama haya aliyatoa Hadhart Khalifa tul Masihi III kama ifuatavyo: Kwamba yeye (Mwana Aliyeahidiwa ra) atajazwa elimu ya ndani na nje, natoa maelezo yake pia kwa kifupi kama ifuatavyo:

Khalifa II ameandika vitabu vingi kuhusiana na Quran tukufu na maelezo yake vinavyoitwa tafsir-e-kabiir. Kuhusiana na kalam ameandika vitabu 10; na kuhusiana na mambo ya kiroho ameandika vitabu 31; na kuhusiana na sira vitabu 13; kuhusu historia vitabu 4. Kuhusu fiqhi vitabu 3, kuhusu siasa vitabu 25, kuhusu siasa za Kashmir vitabu 15, kuhusu historia ya Jumuiya ya Ahmadiyya ameandika vitabu 99.

Khalifa III rh anasema tukijumuisha pamoja vitabu vyote vya madhumuni mbalimbali vinafikia idadi ya 225, na kila aina ya kitabu alichoandika Mwana Aliyeahidiwa ra wapinzani walikiri na kukubali wenyewe kuwa zaidi ya maelezo haya hakuna anayeweza kutoa zaidi. Khalifa III rh anasema haya niliyoyasema ni sehemu ndogo sana ya maandishi yake Mwana huyu Aliyeahidiwara.

Khalifa mtukufu Vatba anasema Allah Amjaalie baraka nyingi maelfu kwa maelfu, nasi Atujaalie kupata uchungu na jazba kwa ajili ya kuieneza dini ya Islam kama alivyojaaliwa Mwana Aliyeahidiwa ra. Nasi tuwe miongoni mwa wale wanaoihudumia dini, na tusiwe miongoni mwa wale wenye kuifedhehesha Jamaati bali tuwe wenye kusonga mbele zaidi na zadi katika kutoa huduma kwa ajili ya dini ya Islam. Amin.

Baada ya hutuba ya Ijumaa Khalifa mtukufu Vatba aliongoza sala ya jeneza la bi Maryamu Elizabeth na la kijana mwenye umri wa miaka 12 aitwaye Jahid Faris.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

JUM.I-JUM.II 1440 AH | FEBRUARI 2020 | TABLIGH 1399 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

.Imesimuliwa na Hadhrat Jabir r.a. kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mfano wa sala tano ni kama mfano wa mto uliojaa maji unaopitia mlangoni pa mmoja wenu, naye anaoga humo kila siku mara tano. (***Muslim***)

Mwana Aliyeahidiwa

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 21/2/2020; baada ya Tashahhud, Taawwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. alisema:

Tarehe 20 mwezi wa Februari inaadhimishwa kama siku ya Mwana Aliyeahidiwa[ra] katika Jumuiya mbalimbali ulimwenguni. Khalifa mtukufu anasema mapema niwajuze watoto na wale wanajumuiya wapya katika Jamaat ya kwamba hatuadhimishi katika siku kuu hii siku ya kuzaliwa kwake Mwana Aliyeahidiwa[ra], badala yake tunaadhimisha kutimia kwa bishara iliyotolewa na Sayidna Masihi Aliyeahidiwa[as] kuhusu ujaji wake na pia siku hii inaadhimishwa kwa sababu ya kutimia ukweli wa dini ya Islam kwa kupitia bishara hii.

Bishara hii ni ishara kubwa kwa wapinzani wa dini ya Islam na kwa fadhili ya Allah ni miaka 134 mpaka sasa imeendelea kung'aa kwa sababu ya ukweli wa dini ya Islam. Kutokana na umuhimu huo kunafanyika maadhimisho katika Jamaat mbalimbali ambamo yale mambo yaliyotimia katika bishara hii huelezwa, lakini hata kwa muda mwingi kabisa bishara hii haiwezi kuelezwa kitimilifu kutimia kwake sembuse katika sala moja.



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa kwa waaminio na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Khalifa mtukufu[atba] anasema kwamba ni bora mimi nieleze kutimia kwa bishara hii kutokana na nukta alizozieleza Mwana Aliyeahidiwa[ra] mwenywe badala ya mimi binafsi kuyaeleza kwa maneno yangu. Kutokana na maelezo hayo msikilizaji atatathmini mwenyewe uzito na umuhimu wa bishara hii na kwa namna ilivyotimia kwa nguvu zote katika dhati ya Mwana Aliyeahidiwa[ra].

Khalifa mtukufu[atba] alisoma maneno ya bishara hii, maneno haya yafuatayo:

Bishara: "Ninakupa Ishara ya Rehema Yangu kwa kuyajibu maombi yako. Nimeyasikia maombi yako na nimekirimu dua zako kwa ukubali Wangu kwa njia ya rehema Yangu na nimeibariki safari yako hii. Ishara ya Qudra na uwezo, ukarimu, ukaribu Nami inatolewa kwako. Ishara ya rehema na ihsani inaletwa kwako na unapewa ufunguo wa ufaulu na ushindi. Amani iko juu yako, ewe mshindi. Hivi ndivyo asemavyo Allah ili kwamba wale wanaotamani uzima waokolewe kutoka mkamato wa mauti na wale waliolala makaburini wafufuliwe na ili kwamba utukufu wa Islamu na heshima ya neno la Mungu Mwenye Enzi idhihirike mbele ya watu na ili kwamba ukweli uwasili na pamoja na Baraka zake zote na uongo utoweke pamoja na nuksi zake zote, na ili kwamba watu waweze kuelewa ya kwamba Mimi ni Mwenye Nguvu, Ninafanya Nipendavyo. Na ili kwamba wawe na yakini ya kuwa Mimi Niko pamoja nawe, na ili kwamba wale wasio mwamini Mungu Mwenye Enzi na wanakana na kukataa dini Yake na kitabu Chake na Mjumbe Wake Mtakatifu, Muhammad Mteule (s.a.w.) wakabiliane na ishara iliyo wazi na ili njia ya wakosefu iweze kubainika."

"Basi furahi ya kwamba utajaaliwa mtoto mwanamume mtakatifu na mzuri, utampokea kijana mwana ambaye atakuwa ni mbegu yako

Endelea uk. 11

KITABU KIPYA

HAJA YA IMAMU



HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD[AS]
Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi

Haja ya Imamu

Kulikuwa na mtu mmoja asiyeelewa hakika ya Uimamu. Kwa kueleza kinaganaga masuala ya Uimamu wa kweli na hakika ya baiati, Seyyidna Ahmad[as] aliandika kitabu hiki kiitwacho ***Dharuratul Imam*** **(Haja ya Imamu)** katika Septemba 1897.

Humo alieleza kwamba Imamu wa zama ni nani na alama zake ni zipi. Vile vile alitaja katika kitabu hiki ubora wa Imamu juu ya wengine wenye kupokea ufunuo na kashfi.

Mwishowe aliandika maelezo ya kesi ya kutozwa kodi.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba Tsh 2,500/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com